*KISWAHILI*

# Mhutasari

## MWONGOZO WA KUSHUGHULIKIA VIKUNDI VILIVYO KATIKA MAZINGIRA HATARISHI (MVMH) NCHINI UGANDA



## UWEKEZAJI KATIKA MISITU NA MAENEO YA HIFADHI KWA UANZISHAJI WA MRADI WA MAZINGIRA SAFI (UMMH-UM)

Wizara ya Maji na Mazingira
Octoba 2020

**Umiliki wa Mradi**: Serikali ya Uganda.

**Mashirika yanayotekeleza:**
Wizara ya Maji na Mazingira (MWE), Wizara ya Utalii, Wanyamapori na Mambo ya Kale (MTWA), Mamlaka ya Wanyama pori ya Uganda (MWU), na Mamlaka ya Taifa ya Misitu (MTM).

**Vyanzo vya Ufadhili:**
Benki ya Dunia (Mfadhili) na Serikali ya Uganda.

**Lengo la Mradi:**
Kuboresha usimamizi endelevu wa misitu na maeneo yaliyohifadhiwa na kuongeza faida kutoka misitu iliyopo katika mandhari lengwa.

**Eneo la Mradi ambapo Batwa wanaishi:**
Wilaya za Kisoro, Rubanda, Kanungu (zinazojumuisha Mbuga za Wanyama za Taifa za Mgahinga na Bwindi, Hifadhi za Misitu za Echuya) na, Wilaya ya Bundibugyo (inayojumuisha Mbuga ya Wanyama ya Semuliki).

**Mwongozo wa Kushughulikia Makundi ya Watu walio katika Mazingira hatarishi**:

Mwongozo wa Kushughulikia Makundi ya Watu walio katika mazingira Hatarishi (MMWMH) ni maelezo ya mikakati na hatua za mradi wa UMMH-UM kuhakikisha kuwa; i) mradi huo unaheshimu utu, haki za binadamu, uchumi, na utamaduni wa Batwa; ii) Batwa kushiriki na kufaidika na utekelezaji wa shughuli za mradi; na, iii) athari mbaya zozote za mradi kwenye Batwa zinapunguzwa vya kutosha.

Shughuli maalumu ambazo zitatekelezwa na Batwa au kutekelezwa kuwasaidia Batwa zitaelezewa katika Mpango wa Usimamizi wa Vikundi vilivyo katika mazingira hatarishi (MUVMH) kwa jamii za Batwa katika / karibu na Hifadhi ya Misitu ya Echuya, Mbuga za Wanyama za Bwindi, Mgahinga Gorilla, na Semliki. MUVMH itaandaliwa kwa kushauriana na Batwa kabla ya kuanza.utekelezaji wa mradi.

**Mchakato wa kuandaa MVMH**:
MVMH hii imeandaliwa na WMM kwa kushauriana na wawakilishi 269 wa Batwa (wanaume 100 na wanawake 169) karibu na Hifadhi za Echuya, Bwindi, Mgahinga Gorilla, na Semuliki; Serikali za mitaa za Wilaya za Kisoro, Rubanda, Kanungu na Bundibugyo na vile vile Mashirika yasiyo ya Serikali (kwa mfano, BMCT, Nature Uganda, PROBICOU) yanayotoa msaada kwa Batwa katika maeneo haya. Mashauriano yalifanywa kati ya tarehe 11 - 15 Februari 2020. Mashauriano yalifanywa

kwa lugha mama / za kienyeji na kuhakikisha kwamba washiriki wa Batwa wanaelewa vizuri malengo ya mradi, mipango ya uwekezaji na utekelezaji pamoja na vifungu vya kuhakikisha ushiriki wa Batwa wakati wa utekelezaji wa mradi.

**Lengo la kuandaa MVMH:**
Lengo la kuandaa MVMH ni kuongoza:

a. Uandaaji na utekelezaji wa hatua za UMMH-UM ambazo zinaweza kuwanufaisha Batwa katika maeneo ya mradi, pamoja na hatua ambazo zinasaidia maendeleo ya njia mbadala za maisha ya Batwa.
b. Mchakato wa upangaji na utekelezaji wa mradi ambao utahakikisha kwamba wanapata idhini ya Batwa kabla ya kuanza kutekeleza shughuli za mradi.
c. Mradi katika kushughulikia masuala yoyote mabaya yanayotarajiwa kuhusiana na Batwa katika eneo la mradi ikiwa ni pamoja na kutambua athari na taratinu za kuzishughulikia.
d. Utekelezaji wa hatua za kukabiliana na kuzuia au kupunguza athari mbaya zozote kwa Batwa.

**MVMH na sera ya kitaifa na mfumo wa sheria:** MVMH inaambatana na sheria za Wazawa wote / makundi yaliyo katika mazingira hatarishi na waliotengwa nchini Uganda kama inavyotolewa chini ya Katiba ya Uganda, sera na sheria nyingine zinazosimamia Fursa Sawa kwa WanaUganda wote, Utamaduni, Ardhi, Wanyamapori, Misitu, Mazingira, Utalii, kati ya mengine.

**Masuala ya kipaumbele kwa Batwa wanaoishi karibu na Mbuga za Mgahinga, Bwindi, Semuliki na Misitu ya Echuya iliyohifadhiwa:** Wakati wa mashauriano na Batwa mnamo Februari 2020, Batwa walionyesha wasiwasi kuhusu masuala yafuatayo;

| Kategoria | Masuala waliyozungumzia |
|---|---|
| Riziki | • Upataji wa rasilimali za misitu kwa ajili ya kujiongezea kipato (kwa mfano, kuweka mizinga ya nyuki ndani ya hifadhi ya msitu, kupanda mianzi kando ya mpaka wa hifadhi ya msitu, upatikanaji wa kuni, n.k.)<br><br>• Upataji wa habari kuhusu Misitu inayolengwa, Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM) na Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali (USR), mipango na shughuli nyingine za maendeleo ambazo zinawaathiri.<br><br>• Usawa wa Batwa kushiriki na kufaidika katika programu za msaada kama ununuzi na ugawaji wa ardhi kwa familia za Batwa; kuongezeka kwa ugawaji wa ardhi kufaidi familia zote za Batwa. |

| | |
|---|---|
| | • Upataji wa huduma za kijamii, haswa elimu na afya.<br><br>• Utaratibu wa kutosha wa kutatua kero zao zinazohusiana na kizuizi cha upatikanaji na matumizi ya rasilimali kutoka Msitu wa Echuya.<br><br>• Kuhifadhi Utamaduni wa Batwa.<br><br>• Kudhibiti shida za wanyama / uvamizi wa mazao. |
| Kushiriki na kufaidika kutokana na mradi | • Kuboresha vinyago vyao pamoja na kuvitafutia soko (kwa mfano, ujenzi wa mabanda na kutenga nafasi za kuonyesha vinyago na bidhaa za ufundi wa Batwa).<br><br>• Upatikanaji wa ardhi na kupata umiliki wa ardhi (umiliki wa ardhi uliosajiliwa).<br><br>• Kupata pembejeo za kilimo (mbegu iliyoboreshwa) na fursa nyingine za kujiingizia kipato.<br><br>• Upatikanaji wa miche ya miti / vifaa vya upandaji (spishi za kibiashara na za asili) na miche ya Mianzi.<br><br>• Kuongeza ushirikiano katika shughuli za usimamizi wa USM / USR na shughuli za USM / USR na upatikanaji wa rasilimali zilizojadiliwa chini ya USM / USR, faida sawa kwa mipango ya Ugawanaji wa Mapato ya Mamlaka ya Wanyamapori Uganda.<br><br>• Kuongezeka kwa ushiriki katika utalii wa mazingira k.m. kufundisha Batwa kushindania fursa za ajira za utalii, kusajili na kutambua vikundi vya Utalii wa Batwa, kuanzisha biashara ya utalii ya Batwa.<br><br>• Shughuli za kuzalisha kipato kwa Batwa kwa mfano, Maduka ya vinyago, ufugaji nyuki |

**Athari hasi zinazoweza kutokana na UMMH-UM kwa Batwa:** Athari mbaya zinazoweza kutokana na mradi huo kwa Batwa zinahusiana na ukweli kwamba mradi unakusudia kuimarisha usimamizi wa maeneo ya misitu yanayolindwa hali itakayoongeza ulinzi wa misitu na utekelezaji wa masharti ya kupata rasilimali za misitu.

Walakini, msaada wa mradi kwa MKM na MWU hautaweka masharti ya ziada kwa Batwa au kuathiri riziki yao.

**Athari chanya za (UMMH-UM) kwa Batwa:** Msaada wa mradi kwa MTM na MWU utasababisha ushirikiano mzuri na Batwa na utoaji wa faida za uhifadhi kupitia; i) upatikanaji wa rasilimali za misitu kupitia Usimamizi Shirikishi wa Misitu (huko Echuya na MTM) na katika Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali katika Mbuga za Wanyama za (Bwindi, Mgahinga na Semuliki); ii) utoaji wa msaada wa riziki kama biashara za msituni (k.v. Ufugaji nyuki), kuongeza thamani kwa vinyago na kukuza shughuli nyingine za Kuingizia kipato kwa Batwa; iii) kushiriki katika utalii wa mazingira; iv) ajira; na, v) kupunguza athari za wanyama kwenye biashara za uwekezaji za Batwa zilizoko nje ya misitu.

**Hatua za kushughulikia athari mbaya:** MVMH huu unabainisha hatua zifuatazo za kuhakikisha kuwa athari hasi kwa Batwa na jamii za karibu zinaepukwa au kupunguzwa.

a. Kuwapa kipaumbele wanajamii na Batwa kwa fursa za ajira katika shughuli zilizo ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa, kama vile; upandaji marejesho, uondoaji wa spishi vamizi, na ujenzi wa miundombinu, utalii, n.k.
b. Kuwajengea Batwa na wanajamii uwezo wa kushiriki kikamilifu na kufaidika katika shughuli za USM / USR, pamoja na kuwashirikisha katika miundo na michakato ya uongozi wa USM / USR.
c. Kudhibiti wanyama na kulinda uwekezaji wa Batwa na jamii katika mazao na mifugo kutoka wanyama wanaowavamia.
d. Kutenga, kuwekea alama na kutangaza mipaka ya Mbuga za Wanyama na Hifadhi ya Misitu.
e. Kukuza uwekezaji ambao unatoa njia mbadala ya rasilimali za misitu (kwa mfano, uanzishaji wa miti) au kutoa maafikiano na matumizi ya rasilimali za misitu kwa kuwasaidia kupata riziki (kwa mfano, bidhaa zisizo za mbao kama uyoga, mimea ya dawa, matunda ya porini, vinyago, n.k. ).
f. Kukuza shughuli za kuzalisha kipato na au kuongeza thamani kwa mazao ya kilimo cha kienyeji.

**Hatua za kuhakikisha kwamba kuna Uhiari wa Awali na Idhini ya Kushiriki:** UMMH-UM inatambua umuhimu wa mashauriano ya kutosha baina ya Batwa na jamii juu ya masuala yote, wakati wa kufafanua faida za mradi na athari zake, na mipango ya utekelezaji wa mradi. Mashauriano yaliyofanywa wakati wa kubuni mradi na utayarishaji wa MVMH yalikuwa hatua za awali. Mashauriano na Batwa katika kuunda MUVMH yatafanyika kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi kwa makusudi kutambua na kuthibitisha shughuli za kipaumbele kwa Batwa na mipango yao ya utekelezaji. Jitihada zitafanywa kuhakikisha kwamba mashauriano yanakuwa ya maana kwa kutoa habari ya

kutosha, sahihi na kwa wakati kwa Batwa kuhusu shughuli za mradi. Hili litafanyika kabla ya mikutano ya mashauriano, kuwahamasisha kuhusu shughuli za mradi, kuwashirikisha katika kupanga na kuwapa maoni juu ya MUVMH.

**Kuendeleza MUVMH**: Mipango ya Usimamizi wa Vikundi vilivyo katika Mazingira hatarishi vya Batwa itaanzishwa kwa kila eneo lililohifadhiwa. Kwa jumla VMGMP vinne (4) zitaanzishwa. MUVMH itaelezea shughuli ambazo zitapewa msaada na mradi huo pamoja na mipango ya utekelezaji na ufadhili. MUVMH itafadhiliwa kivyake.

**Jitihada za kushughulikia malalamiko juu ya UMMH-UM:**

Njia ya kushughulikia maswala halali ya watu walioathiriwa na mradi, pamoja na Batwa itatengenezwa hapo awali kabla ya utekelezaji wa mradi na kutumika wakati wa utekelezaji wa mradi. Utaratibu huu utatoa njia rasmi kwa Batwa na vikundi vingine vinavyoathiriwa au wadau kushirikisha mradi huo kuhusu masuala tofauti au athari ambazo zitakuwa hazijashughulikiwa. Mradi utahamasisha Batwa na watu wengine watakaoathiriwa na mradi kuhusu utaratibu huu, taratibu za matumizi yake na kutoa maoni kwa walalamikaji. Inatarajiwa kuwa utaratibu huo utafanywa rasmi lakini rahisi kwa kutumia miundo ya kusuluhisha mizozo na kuunda michakato au kupitia miundo ya utatuzi wa malalamiko katika ngazi za vijiji au jamii haswa kwa mradi huu.

# INVESTING IN FORESTS AND PROTECTED AREAS FOR CLIMATE SMART DEVELOPMENT (IFPA-CD) PROJECT

ifpa-cd
Invest in Nature. Secure the Future.



UWA
Conserving for Generations

NFA
NATIONAL FORESTRY AUTHORITY




***Contacts***
Ministry of Water and Environment
Plot 3 – 7 Kabalega Crescent Road, Luzira
P. O. Box 20026 Kampala, Uganda
Tel: +256 417 889 400
Email: mwe@mwe.go.ug
Website: mwe.mwe.go.ug